

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**  
**MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA**  
**TAREHE 1-3/12/2016**

**MAHUDHURIO**

1. MH. ERICK E. NKLAMACHUMU	MWENYEKITI
2. BW. AIDAN BAHAMA	KATIBU (DED)
3. MH.JOHN M. SHIM I'MANA	MJUMBE
4. MH.MKUBILA S. SOUD	MJUMBE
5. MH.ADRONIZI E. BURINDOLI	MJUMBE
6. MH.OLIPA A. BUGOKE	MJUMBE
7. MH.KHAMIS B. HAMADI	MJUMBE
8. MH.ROMAN MITABARO	MJUMBE
9. MH.JUSTUS K. MASUMO	MJUMBE
10. MH.DAVID I BUZUTU	MJUMBE
11. MH.GWIHANGWE M. EDWARD	MJUMBE
12. MH. VAILETH MADENDE	MJUMBE
13. MH.SAID R. SOUD	MJUMBE
14. MH.ZAWADI D. COSMAS	MJUMBE
15. MH.WILBARD J.BAMBARA	MJUMBE
16. MH.GWASSA NTUNGIYE	MJUMBE
17. MH. SUZANA N. BAHATI	MJUMBE
18. MH. FIDEL F. NDANGWA	MJUMBE
19. MH.MUKIZA S. BYAMUNGU	MJUMBE
20. MH.NZEYE LEONARD	MJUMBE
21. MH.SENTORE J. MIBURO	MJUMBE
22. MH.PHILBERT M KIIZA	MJUMBE
23. MH.MUGATA M. ELIAS	MJUMBE
24. MH.GEORGIA MUNYONYELA	MJUMBE
25. MH.KAGOMBA S. GEORGE	MJUMBE
26. MH.LAURENT J. MUSUNGARERE	MJUMBE
27. MH.CATHERINE EDWARD	MJUMBE
28. MH.REHEMA S. RAMADHANI	MJUMBE
29. MH.SAFARI N. BANIGWA	MJUMBE
30. MH. EDITHA MWINURA	MJUMBE

WAJUMBE WASIOHUDHURIA-Kwa taarifa

1. MH ALEX GASHAZA(MB)

**WAJUMBE WAALIKWA**

1. MH. LT. CLO. MICHAEL MNTENJELE	MKUU WA WILAYA
2. BW. ELIAS ZEPHANIA	MWANDISHI WA HABARI, RK
3. BW. HUDSON BAGEGE	MWENYEKITI- CCM(W)
4. BW. JACOB MAKUNE	KATIBU- CCM (W)

**WATAALAM WALIOHUDHURIA:**

1. BW. BIGAMBO AMOS
2. BW. MASOUD ABDALLAH
3. BW. MOSES KICHOGO
4. BW. BULILO MUSOMBWA DEYA
5. BW. F.M KAPAMA
6. BW. JUMANNE MAGUNGU
7. BW. JULIUS ERNEST
8. BW. THEONEST THADEO
9. BW. MORIS MOMBIA
10. BW. PASTORY M. MSABILA
11. BW. CONSTANTINE MUDENDE
12. BW. FIDELIS MALIMBU
13. BW. SANGATATI JOSEPHAT
14. BI. SAKINA CHAMITI
15. BW. HERMAN HUME
16. BI. PERPETUA RULIMBIYE
17. BW. GIDEON MWESIGA
18. BI. BETTY S. MUNUO
19. BW. SERIALIS ANTONY
20. BW. TOBA A. MUHINA
21. BW. STEPHANO NGULINZIRA
22. BW. NELSON RUFANO
23. BW. FREDRICK KAKURU
24. BW. MICHAEL NDYAMUKAMA
25. BI. BETTY S. MUNUO
26. BW. SUBIRA V. MANYAMA
27. BI. REINFRIDA ANZIGARY

AFISA MIPANGO (W)  
MWEKA HAZINA(W)  
AFISA HABARI  
MWANASHERIA WA (W)  
MKAGUZI WA NDANI(W)  
KAIMU MUHANDISI WA MAJI  
KNY AFISA TARAFYA NYAMIHAGA  
KAIMU AFISA TARAFYA KANAZI  
KAIMU AFISA TARAFYA RULENGE  
AFSA TARAFYA MURUSAGAMBA  
KAIMU AFISA KILIMO WILAYA  
K/AFISA ELIMU SEKONDARI(W)  
K/AFISA MIFUGO NA UVUVI(W)  
MRATIBU WA TASAF  
AFISA MAENDELEO YA JAMII(W)  
KAIMU AFISA UGAVI (W)  
AFISAELIMU YA MSINGI(W)  
AFISA ARDHI(W)  
TEO-RULENGE  
AFISA MAZINGIRA(W)  
AFISA MABORESHO  
KAIMU MGANGA MKUU(W)  
KAIMU AFISA UTUMISHI(W)  
KATIBU TSD(W)  
AFISA ARDHI NA MALIASILI (W)  
KAIMU MUHANDISI UJENZI(W)  
KATIBU WA KAMATI (H/W)

## **MUHT NA 1/2016/2017: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwasalimia wajumbe na kumkaribisha Mwenyekiti aweze kufungua kikao. Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwasalimia wajumbe na kumkaribisha Mwenyekiti aweze kufungua kikao. Mwenyekiti alianza kwa kuwasalimia wajumbe na kueleza kwamba kikao kinachofanyika tarehe 2/12/2016 agenda zitakazojadiliwa ni pamoja na kuwasilishwa kwa taarifa za kata na kikao cha tarehe 3/12/2016 agenda zingine za kikao zitaendelea kujadiliwa , aidha aliishukuru Kamati ya Maadili pamoja na Mkurugenzi Mtendaji kwa kuwezesha kila Mheshimiwa Diwani kupatiwa eneo lake la kukaa wakati wa kikao na kuondoa vurugu zilizokuwa zinajitokeza, pia aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kutumia muda mchache katika kujadili agenda kwa sababu inafahamika kuwa miradi mingi ya maendeleo hajatekelezwa kwa sababu fedha zake hazijaletwa. Kikoa kilifunguliwa saa 3.37 asubuhi.

## **MUHT NA 2/2016/2017: KURIDHIA AGENDA**

Wajumbe walizipokea agenda na kuridhia.

## **MUHT NA 3/2016/2017: TAARIFA ZA KATA ROBO YA I, 2016/17**

### **KATA YA BUKIRIRO**

Kata ya Bukiriro imeundwa na vijiji 4, ina kaya 5048 na watu wapatao 21713 kati yao wanaume 10589 na wanawake 11124.

Vikao vya ulinzi na usalama vilifanyika 3, Vikao vya ulinzi na usalama vilifanyika kwa 100%, vikao vya VDC vilifanyika 2 sawa asilimia 95%, Mikutano mikuu ilifanyika kwa asilimia 100% kwa vijiji vyote vilivyoko katani, kwa kata ya Bukiriro vikao vya ulinzi na usalama vilifanyika vyote kwa 100%, vikao vya Kamati za maendeleo ya kata WDC vilifanyika vyote sawa 100%.

Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo, ujenzi wa nyumba za waalimu 1:6 mradi wa benki ya dunia ujenzi umefikia ya boma kukamilika, ujenzi wa madarasa 4, vyoo matundu 8, vyoo vya waalimu matundu 2 fedha iliyotumika ni Tshs. 105,948,720.00, Mradi wa TASAF III kunusuru kaya maskini 145 Mumuhamba fedha ilitolewa kuwapa maskini jumla ya Tshs. 14,352,090, kwa kaya 137 za kijiji cha Murulama Tshs.17,8047,804,977.00/=, Kijiji cha Nyabihanga kaya maskini 125 fedha ilitolewa ilikuwa Tshs. 13,326,766.06/=.

Fedha za ruzuku katika shule za msingi, Bukiriro mapato Tshs.1,235,338.79, Rubanga Tshs. 845,730.05 Nyabihanga Tshs. 1,269,798.41, Mumuhamba Tshs. 985,789.69/=, Mubwilinde Tshs1,639,200.54/= Kigarama Tshs. 2,210,010.99/=, Rulama Tshs. 1,367,561.27/=.

Fedha za ruzuku shule ya sekondari Bukiriro mapato yalikuwa Tshs. 3,550,241/=

Mapato yaliyotokana na zahanati ya Bukiriro H/C salio lilikuwa Tshs. 5,243,800.00,

### **KATA YA RUSUMO**

Fedha zilizopokelewa katika shule za msingi Kaburanzwili, Kasharazi, Nyakahanga, R/Magereza robo ya I, Rusumo B sekondari Julai mpaka Septemba jumla Tshs. 2,791,000/=

Vikao vya kisheria vilivyofanyika, Kamati ya Maendeleo ya kijiji kilifanyika kikao 2, kikao,

Halmashauri ya kijiji cha Rusumo hawajafanya kikao, Halmashauri ya kijiji cha kasharazi, Rusumo na Mshikamano jumla vilifanyika vikao 9, mikutano mikuu ya kijiji cha Rusumo, Mshikamano na Kasharazi jumla ilifanyika mkutano 9 tu, Halmashauri ya kijiji cha mshikamano vilifanyika vikao 3, Mikutano mukuu katika kijiji cha Mshikamano, Kasharazi na Rusumo iliyofanyika jumla ilikuwa 3

Shughuli za kiuchumi, wakazi wanajishughulisha na kilimo, biashara, usafirishaji na ufugaji

Hali ya ulinzi na usalama ni nzuri kwani viongozi wanafanya kazi kwa ushirikiano.

Zahanati ya Mshikamano kutokuwa na Mganga Mfawidhi, wanafunzi kutembea umbali mrefu, Barabaraya Rusumo magereza kuharibika na kusababisha kutopitika .

### **KATA YA MURUSAGAMBA**

Vikao vya kisheria vilivyofanyika Julai hadi Septemba 2016, Kamati ya Maendeleo ya kata (WDC) kikao 1, ulinzi na usalama Magamba 3, Ntanga 3 Murusagamba 3, Serikali ya kijiji Magamba 3, Ntanga 3 na Murusagamba 3 mikutano mikuu ya vijiji ilifanyika mikutano 4.

Mapato yaliyotokana na soko pamoja na nyumba ya kulala wageni jumla Tshs. 1,600,000/=, Mapato ya vijiji Murusagamba, Ntanga na Magamba jumla Tshs. 8,126,090.91/=

Fedha za ruzuku zilizopokelewa shule ya msingi Murugunga Tshs. 1,812,000/=, Ntanga Tshs. 1,140,000/=, Murusagamba 3,310,000.00.

Mapato yaliyopokelewa katika shule sekondari jumla Tshs. 22,740,000/=  
Hali ya ulinzi na usalama ni shwari.

### **KATA YA NTOBYE**

Vikao vya kisheria vilivyofanyika katika Kata ya Ntobeye vikao vya VDC kijiji cha Chivu 2, Ntobeye 3, Runzenze 3, Kigina 1, Vikao ngazi ya Kitongoji, Chivu 8, Ntobeye 14, Runzenze 13 na kigina 0, Mikutano mikuu iliyofanyika jumla ilikuwa 4

Mapato na matumizi yaliyotaikana katika kijiji cha Chivu Tshs. 207,238.00, matumizi 2015,414/=, Ntobeye Tshs. 209,300/= matumizi 58,800/=, Runzenze Tshs. 850,000/= matumizi Tshs. 850,000/=, Kigina Tshs 975,000/= matumizi Tshs. 635,000.

Mapato (fedha za ruzuku) yaliyopatikana Julai-Septemba katika shule 5 za msingi Ntobeye, Chivu, Nyakariba, Murukagati, na Kigina jumla Tshs. 6,308,000/=

Fedha za ruzuku katika shule za Sekondari mapato ni Tshs.2,216,000/= fidia ya ada Tshs. 2,328,000/= jumla Tshs. 4,544,000.00/= matumizi Tshs.2,611,700/= baki Tshs. 1,932,300/=

Mapato zahanati ya Ntobeye michango ya CHF, UF na NHIF zilizopokelewa papo kwa papo jumla Tshs. 605,650.00, Mapato zahanati ya Chivu michango ya CHF, UF na NHIF zilizipokelewa papo kwa papo jumla Tshs. 866,470.00/=,

Shughuli za kiuchumi katika Kata ya Ntobeye ni kilimo na ufugaji

Kata ya Ntobeye ilibahatika kuwa mionganoni mwa kata zilizowekwa kwenye mpango wa TASAF III, vijiji 3 vilihusishwa na mpango huu, vijiji hivyo ni Runzenze walipata Tshs. 3,498,000.00, Kigina walipata Tshs. 10,003,659.09 na Ntobeye walipata Tshs. 19,144,831.82/= Katika kijiji cha Ntobeye TASAF III ina mpango wa kuanzisha mradi wa uchimbaji wa visima 7 vyenye mita na ujazo 72 pia mradi wa upandaji wa vitalu vya miti katika eneo kubwa lenye hekta 19.7

Miradi ya Maendeleo katika Kata ya Ntobeye, kununua seti za vifaa vya chanjo kijiji cha Runzenze, kununua vitendanishi vya maabara zahanati ya Chivu, kuanza ukarabati wa mradi wa maji chivu A na B, kuhamasisha uzalishaji wa mnazao ya kilimo ya aina zote, kuanzisha shamba moja la mfano la kahawa, ujenzi wa matundu ya vyoo 5 katika shule ya msingi Chivu na 5 katika shule ya msingi Murukagati, ujenzi wa bweni 1 shule ya sekondari Ntobeye, kufanya matengenezo ya kawaida barabara ya Chivu-Ntobeye-Nyakiziba, kufanya matengenezo ya kawaida katika barabara ya Murugwanza-Runzenze, kufanya matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Mukididili-Chivu-Kigina shule ya msingi km 8

Changamoto zilizoko katika Kata ya Ntobeye, upungufu wa miundo mbinu kama nyumba za waalimu, madarasa, madawati na matundu ya vyoo, upungufu wa waalimu wa masomo ya hisabati na sayansi, mwitikio mdogo wa wananchi kuijunga na mfuko wa afya ya jamii (CHF), Kutoletwa kwa fedha za miradi ya maendeleo.

### **KATA YA KIBIMBA**

Vikao vya kisheria, WDC vilifanyika kikao 1, Halmashauri ya kijiji vilifanyika vikao 11, kimoja hakijafanyika, Mikutano ya vitongoji ilifanyika 15 kati ya 60, mikutano mikuu 4.

Mapato na matumizi, fedha zilizopokelewa kupitia michezo Tshs. 323,800, Kununua vifaa vya madarasa Tshs. 917,400, ukarabati wa majengo na vifaa 971,400, Mitiani ya Ndani Tshs. 585,200, kwa matumizi ya utawala Tshs. 386,200.

Fedha zilizowasilishwa Halmashauri toka mwezi Julai hadi Septemba BUH Tshs. 331,500, Kilimo Tshs. 202,500, KUMUT Tshs. 52,500, na RUGANZO 3000/=

Mapato ya zahanati CHF Rugazo, Tshs. 130,000/=, Kumtana Tshs. 100,000/= Mayenzi Tshs. 70,000, na Buhororo Tshs. 1,627,472/= UF Ruganzo 130,000/=, Kumtana 95,000/= Mayenzi 80,000/= na Buhororo hakuna. Mapato yaliyotokana na vijiji vya Buhororo, Mayenzi, Kumtana na Ruganzo Jumla 1,280,000/=

Mapato yaliyopokelewa katika shule ya sekondari Kibimba Tshs. 2,850,000/=

### **KATA YA MABAWE**

Vikao vya kisheria, Kamati ya maendeleo ya Kata kilifanyika kikao 1, Kamati ya ulinzi na usalama ya Kata vilifanyika vikao 3, ngazi ya vijiji Murugina Halmashauri kuu ya kijiji vilifanyika vikao 3, mkutano mkuu 1, Mukaliza Halmashauri ya kuu ya kijiji 3, mkutano

mkuu 1 na kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji 3, Kumwuzuza Halmashauri kuu ya kijiji 3, mukutano mkuu 1, kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji 3, Murugarama Halmashauri ya kuu ya kijiji mikutano 2, mikutano mikuu 2, Kamati ya ulinzi na usalama 3, Muhweza Halmashauri kuu ya kijiji 3, mukutano mkuu 1, kamati ya ulinzi na usalama 3.

Ngazi ya kitongoji mikutano mikuu iliyofanyika ilikuwa 27 kati ya 66, kamati ya ulinzi na usalama mikutano iliyofanyika 54 ambayo haijafanyika 12

Hali ya ulinzi na usalama ni nzuri kwa robo ya I licha ya kuwepo kwa wizi mdogo mdogo wa mifugo.

Mapato yaliyokusanywa, ushuru wa masoko, ushuru wa mazao , faini toka Baraza la Kata, ada ya ukaguzi wa vyama Tshs. Jumla yalikuw Tshs. 7,553,000/=

### **KATA YA NYAKISASA**

Mikutano ya kijiji ngazi ya WDC vikao vya ulinzi na usalama vilifanyika vikao 5, Serikali ya Kijiji mikutano mikuu katika kijiji cha Kashringa 1, Kumugamba 1, Nyamahwa 1, kigoyi mikutano 1, Halmashauri ya vijiji, kijiji cha Kashringa 1 Kumugamba 1, Nyamahwa 1, Kigoyi 1.

Mapato ya shule za msingi Kata ya Nyakisasa jumla ya fedha zilizoko benki ni Tshs. 1,774,849.88/=

Mapato yaliyokusanywa kutokaa na gulio jumla Tshs. 600,000/=, ushuru wa mazao haukukusanywa.

### **KATA YA BUGARAMA**

Vikao vya kisheria, kijiji cha Bugarama VDC mikutano 2, mikutano mkuu 1, Rwinyana VDC mikutano 2 mikutano mkuu 1, Mumiramira VDC mikutano 1, mikutano mkuu 1,Kamati ya Maendeleo ya Kata ulifanyika mikutano 1, mikutano mikuu ilifanyika kwa 100%.

Mapato yalikusanywa na kuwasilishwa Halmashauritoka mwezi Julai hasi Septemba 2016 jumla yalikuwa Tshs. 5,810,800/=

Michango ya CHF kwa kipindi cha mwezi Aprili mpaka Juni katika zahanati ya Bugarama Tshs. 313, 000/= na Mumiramira jumla Tshs. 750,000/=

### **KATA YA KANAZI**

Vikao vya kisheria vilivyofanyika Kamati ya maendeleo ya Kata (WDC) kikao 1 sawa na 100%, kamati ya ulinzi na usalama Kata vilifanyika vikao 3, Serikali ya Kijiji vikao 17, Kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji vikao vilivyofanyika ni 17, Mikutano mikuu ya vijiji vilifanyika vikao 6, Mikutano mikuu ya vitongoji vilivyofanyika jumla vilikuwa ni 60.

Mapato na matumizi katika kata ya Kanazi, soko la Kanazi Julai hadi Septemba, 2016 walikusanya jumla ya Tshs. 10,160,000/=, makusanyo ya zahanati kata ya Kanazi kwa michango ya huduma ya papo kwa papo Tshs. 100,000/=, na CHF Tshs. 10,000/= zahanati ya Katerere Papo kwa papo Tshs. 122,000/= CHF Tshs. 390,000/= zahanati ya Kabalenzi

hakuna makusanyo yaliyofanyika, zahanati ya Mukarehe huduma ya papo kwa papo Tshs. 90,000/= NHIF Tshs. 87,455/= na CHF Tshs. 210,000/=

Mapokezi ya fedha za ruzuku kwa kila shule za msingi Nyarusange Tshs. 542,000/=, Mukirehe Tshs. 610,000/=, Remela Tshs. 382,000/=, Mukarehe Tshs. 506,000/=, Kanazi Tshs. 742,000/= Kabalenzi Tshs. 434,000/=, Mukibogoye Tshs. 942,000/= Katerere Tshs. 699,000/=

Malipo ya fedha za TASAF III katika kijiji cha Mukarehe Tshs. 3,401,000/=, Mukibogoye Tshs. 3,994,954.55/= Mukarehe Tshs. 4,381,431.82 na Kabalenzi Tshs. 3,140,636.36/=

### **KATA YA KIBOGORA**

Vikao vya kisheria ngazi ya Vitongoji hufanyika hadi ngazi ya Kata inafanyika na Mihtasari inawasilishwa kwenye ngazi ya Kata hadi ngazi ya Halmashauri ya Wilaya.

Mapato na matumizi yaliyotokana na ushuru wa mazao na ushuru wa soko, ushuru wa mazao Tshs. 679,500/= ushuru wa soko Tshs. 200,000/= ukaguzi wa nyama Tshs. 29,000/=

Mapato yanayotokana na ushuru wa mazao jumla Tshs. 679,500/=, Ushuru wa soko Tshs. 200,000/=, Ukaguzi wa nyama Tshs. 29,000/= ushuru wa vibanda Tshs. 110,000/=

Mapato yanayotokana na CHF Kihinga Tshs. 280,000/= malipo ya papo kwa papo Tshs 16,000/= Mfuko wa CHF katika zahanati ya Nyalurama Tshs. 130,000, malipo ya papo kwa papo Tshs. 56,000/=

Fedha za ruzuku zilizopokelewa katika shule ya msingi Nyarulama Tshs. 1,168,000/=, shule ya msingi Kihinga Tshs. 1,468,000/=, shule ya msingi Nyarukubala Tshs. 900,000/= na mapato yaliyopokelewa shule ya sekondari Kibogora yalikuwa Tshs. 2,946,000/=

### **KATA YA MUGOMA**

Vikao vya kisheria, WDC kilifanyika kikao 1, VDC vimefanyika 15, Halmashauri ya kijijivikao 65 katika vijiji vyote 5, Mugoma, Shanga, Mukikomero, Muruvyagira na Mubuhenge.

Mapato na matumizi, ushuru wa beria Tshs. 3,120,500/= ushuru wa soko Tshs. 748,000/=, ushuru wa machinjio Tshs. 32,500/=.

Fedha za ruzuku kwa shule za msingi Mugoma mwezi Julai hadi Septemba Tshs. 586,000/=, Mubuhenge Tshs. 792,000/=, Mugikomero Tshs. 244,000/=, Mukagugo Tshs. 514,000/= na Shanga Tshs. 961,400/=.

Shule ya sekondari Mugoma mapato ni Tshs. 3,164,000/=, Shule ya sekondari Muruvyagira Tshs. 2,499,000/=

Fedha za kunusuru Kaya maskini TASAF III jumla ya kaya 396 walinufaika katika vijiji vya Shanga kaya 103 walipatiwa jumla ya Tshs. 18,667,000/=, Muruvyagira kaya 139 walipatiwa jumla ya Tshs. 21, 626,958.00/=, Mugikomero kaya 70 walipatiwa jumla ya Tshs. 13,545,907.00/=-, na Mubuhenge kaya 84 walipatiwa jumla ya Tshs. 11,536,000/=.

## **KATA YA NGARA MJINI**

Fedha za elimu bure zilizoletwa katika shule za sekondari kuanzia mwezi Julai mpaka Septemba zilikuwa kama ifuatavyo; Ngara mjini Tshs. 5,220,000/=, Murgwanza Tshs. 1,745,910.14/=, shule za msingi zina jumla ya waalimu 174, na sekondari waalimu 60 wameajiriwa na Serikali na waalimu 25 ni ajira binafsi kwa ajili ya shule ya msingi na awali ya NAPS waalimu 13 na waalimu 12 katika shule ya sekondari ya Mchungaji Mwema.

Fedha zilizopokelewa kwa shule za msingi 6 Ngara MJini. Murgwanza, Nakatunga, Mukididili, Nyamiaga, na Mubinyange jumla Tshs. 14,719,000/=

Vikao vya kisheria vilivyokwisha, kilifanyika kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango Mji, na vingine vilishindikana kwa sababu ya ukosefu wa fedha za uendeshaji wa vikao hivyo.

Changamoto zilizoko katika shule za msingi upungufu wa matundu ya vyoo, madarasa na madawati, changamoto zilizoko katika shuleza sekondari ni pamoja na upungufu wa viti na meza, matundu ya vyoo, miundo mbinu ya maji, upungufu wa waalimu wa sayansi.

## **KATA YA MURUKULAZO**

Vikao vya kisheria kamati ya maendeleo ya Kata kilifanyika kikao 1, Ulinzi na usalama vilifanyika vikao 3, Halmashauri ya kijiji vilifanyika vikao 6 kwa kila kijiji,

Vyanzo vya mapato katika Kata ya Murukulazo ni pamoja na soko la Murunyinya na ushuru wa nyama, kuna vyanzo vingine ambavyo haviko hai kama vile mnara wa simu, mchanga na mawe.

Hali ya ulinzi na usalama ni shwari changamoto zipo ndogondogo.

## **KATA YA RULENGE**

Vikao vya kisheria vilifanyika kwa kuzingatia ratiba zake kama vile mashina, mitaa pamoja na Mamlaka.

Mapato yaliyopatikana toka mwezi Julai-Septemba 2016 kutoka katika vyanzo mbalimbali kama vile soko, mazao mchanganyiko, ushuru wa vibanda, ushuru wa gesti, ushuru wa mchanga, ushuru wa Tax, ushuru wa machinjio na ushuru wa mnada jumla yalikuwa ni Tshs.21,788,500/=

Hali ya ulinzi na usalama ni nzuri hakujatokea tatizo lolote la uvunjifu wa amani.

## **KATA YA KEZA**

Vikao vya Halmashauri ya Vijiji vilivyofanyika, Keza vikao 3 Kazingati 3. Mikutano mikuu iliyofanyika Keza 1, Kangati hawakufanya mkutano. Vikao vya ulinzi na usalama Keza mikutano 3 na kazingati 3, Kamati ya maendeleo ya Kata (WDC) keza vilifanyika vikao 1.

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Kata ya Keza, Kijiji cha Keza ujenzi wa

matundu 4 ya vyoo vya Murusagamba shule ya msingi Keza, utengenezaji wa madawati 25 na kukarabati wa madawati 5, Kijiji cha Kazingati ujenzi wa ofisi ya kijiji Kazingati na utengenezaji wa madawati 29 yamekamilika, Kibirizi madawati 12 shule ya msingi Rwenzaza 7, utengenezaji wa madawati 50 mapya yanatengenezwa ambapo tayari 30 yamekamilika.

### **KATA YA NYAMAGOMA**

Vikao vya kisheria, vikao vya kijiji Murubanga 3, Kumubuga 1, Kititiza 3 na WDC 1, Mikutano mikuu ya kijiji Murubanga 1, Kumubuga 0, na Kititiza 1 Mikutano ya Kitongoji Murubanga 15 na Kumubuga 1, Kititiza 3 na vikao vya ulinzi na usalama Murubanga 3, Kumubuga 0, Kititiza 3, WDC 3.

Mapato kwa kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, ushuru wa beria Tshs.243,900/= na ushuru wa mazao mbalimbali Tshs. 684,000/= zote ziliwasilishwa Halmashaur ya Wilaya

Fedha za ruzuku katika shule za msingi shule ya msingi Kahama Tshs. 1,190,252.11, Kumubuga Tshs. 1,689,056.52 na Kititiza mapato Tshs. 1,024,000/=

Fedha za TASAF III zilizotolewa kunusuru kaya maskini Robo I, kijiji cha Murubanga Tshs. 2,808,159.09 na Kumubuga Tshs. 3,010,454.55 kwa walengwa wa TASAF.

Michango ya zahanati papo kwa papo Tshs. 40,000/=, CHF Tshs. 42,000/=

### **KATA YA MBUBA**

Vikao vya kisheria vilivyofanyika, vikao vya WDC vilifanyika 1, Vikao vya VDC vilifanyika 5, Mikutano ya kijiji ilifanyika 1, vikao vya ulinzi na usalama kilifanyika 1 katika kijiji cha Mbuba.

Mapato na matumizi ya vijiji, kijiji cha kanyinya mapato yalikuwa Tshs. 275,000/= Kijiji cha Mbuba mapato yalikuwa Tshs. 205,000/= kijiji cha Kumwendo mapato yalikuwa Tshs. 215,000/= Kijiji cha Ruhuba mapato yalikuwa ni tshs. 111,000/=

Michango ya maabara katika vijiji vyote 3 vya Mbuba, Kumwendo na Ruhuba yalikuwa ni Tshs. 992,000/= matumizi Tshs. 905,000/= salio lililobaki 87,000/=

Mapato katika zahanati ya Kanyinya CHF, Tshs.290,000/= papo kwa papo Tshs. 150,000/=, zahanati ya Mbuba CHF 580,000/= papo kwa papo 148,000/=

Mapato ya soko jumla Tshs. 1,268,500/= na zote ziliwasilishwa Halmashauri.

Fedha za capitation katika shule ya sekondari Ndomba jumla ya fedha iliyoletwa ni jumla Tshs. 7,154,000/=

Fedha za Capitation katika shule za msingi kanyinya fedha iliyoletwa jumla ilikuwa ni Tshs. 872,000/= Mbuba Tshs. 982,000/=, Ruhuba Tshs. 744,000/= na Kumwendo Tshs. 912,000/=

## **KATA YA KIRUSHYA**

Vikao vya kisheria ngazi ya VDC vikao 12 katika vijiji vyote Mwivuza 3, Murutabo 3, Kasange 3 na Kirushya 3., mikutano mikuu 4, na Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) kikao 1 katika robo ya I 2016/17

Mapato yaliyokusanywa na kuwasilishwa Halmashauri yalikuwa Tshs. 165,000/= Mapato yanayotokana na mradi wa kunusuru kaya maskini TASAF III, kaya maskini zipo 111 fedha iliyotolewa malipo ya mwezi Julai mpaka Septemba, 2016 Tshs. 4,080,000/=, Kijiji cha Murutabo kaya maskini zipo 97 malipo ya fedha yaliyofanyika toka mwezi Mei mpaka Juni ni Tshs. 3,388,000/=, Mwivuza Tshs. 5,568,000/=

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ujenzi wa maabara shule ya Sekondari Kirushya zimekusanywa Tshs. 142,000/=.

Hali ya ulinzi na usalama katika Kata ya Kirushya ni nzuri.

## **KATA YA KASULO**

Mapato katika Kata ya Kasulo kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato toka mwezi Julai-Septemba jumla yalikuwa Tshs. 39,129,700/= makusanyo yam nada wa ng'ombe toka mwezi Julai hadi Septemba yalikuwa ni Tshs. 7,970,000/=

Taarifa ya mapato na matumizi ya michango ya wananchi wa kijiji cha Kasulo jumla yalikuwa Tshs. 6,530,000/=, matumizi yalikuwa ni Tshs. 4,688,100/= na salio lililobaki ni Tshs. 1,841,900/=

Fedha za ruzuku zilizopokelewa katika shule za msingi ziliikuwa kama ifuatavyo; Kasulo S/M Tshs. 470,000/=, Njiapanda S/M Tshs. 2,204,000/=, Kapfuha S/M Tshs. 208,000/=, Kumnazi S/M Tshs. 1,286,000 /=, Kamuli S/M Tshs. 364,000/= Kabaheshi S/M Tshs. 60,377.63, Ngoma S/M Tshs. 452,000/= Jumla Tshs. 5,044,377.63/=

Fedha zilizopokelewa katika shule ya sekondari za Kasulo; Lukole sekondari Tshs. 54,723,000/= Rusumo A Tshs. 4,033,325/= Michango ya CHF, NHIF na malipo ya papo kwa papo katika kituo cha afya Lukole jumla zilikusanywa Tshs. 3,158,000/= mapato yanayotokana na maji bubujiko Tshs. 45,415,780/= matumizi Tshs. 35,030,270/= salio lililobaki Tshs. 10,385,510/=

## **KATA YA KABANGA**

Miradi ya maendeleo iliyotekelawa, utengenezwaji wa madawati 116 kwa kata nzima ambapo jumla ya Tshs. 4,640,000/= zinahitajika na madawati 61 yenyewe thamani ya Tshs. 610,000 yalikarabatiwa katika kipindi cha robo ya kwanza, jumla ya michango iliyochangwa ilikuwa ni Tshs. 5,20,000/=, mradi wa matundu 10 ya vyoo na vyumba 2 vya madarasa katika shule ya sekondari Nyabisindu zenyewe thamani ya Tshs. 94,736,300/= mradi wa ujenzi wa maabara mradi huu umekamilika isipokuwa kuna mapungufu ya miundo mbinu.

Ujenzi wa soko la kimataifa Nzaza-Kabanga umekwama kabisa na hakuna maelezo ya kina

ya hatma ya mradi huo, fance ilianguka na bati zinaendelea kuharibika na kuna walinzi 3 wanaolinda eneo hilo hawajalipwa mashahara kwa muda mrefu. Na mradi wa ujenzi wa maabara.

Mapato na matumizi ya kata ya Kabanga, fedha zilizokusanya katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba zilikuwa ni Tshs. 24,456,450/= ikijumlishwa na mapato mengine ya nje jumla ya makusanyo ni Tshs. 153,623,140.80 matumizi yalikuwa ni Tshs. 81,151,302.60 na kubaki Tshs. 72,471,838.20

Hali ya ulinzi na usalama ni nzuri na vikao vyote vya ulinzi na usalama vilifanyika kulingana na ratiba.

### **KATA YA NYAMIAGA**

Vikao vya kisheria vilivyofanyika katika Kata ya Nyamiaga, Kamati ya Maendeleo ya Kata vilivyofanyika ni 1, Halmashauri ya maendeleo ya vijiji vilifanyika vikao 10, havikufanyika vikao 14, Vikao vya kitongoji vilifanyika vikao 32, havikufanyika vikao 88.

Mapato na matumizi katika kata ya Nyamiaga, mapato yanayotokana na michango ya wananchi Tshs. 2,290,000/= matumizi yaliyofanyika ni Tshs. 1,847,000/= baki 443,000/=

Mapato yanayotokana na zahanati ya Nterungwe makusanyo yalikuwa Tshs. 1,100,000/=.

Fedha za capitation katika shule za msingi Mumiterama Tshs. 840,856.51, Mugasha Tshs. 807,919.03, Kumuyange Tshs. 1,011,959.12

### **KATA YA MUGANZA**

Mapato na matumizi ya fedha za ruzuku katika shule za msingi Muganza, Rusengo, Nyakafandi, Mukubu, Rwimbogo, Musaza na Ngeze mapato Tshs. 12,570,500/= matumizi Tshs. 11,375,500/=salio lililobaki Tshs. 1,195,000/=

Vikao vya kisheria vilivyofanyika VDC Mukubu vilifanyika 2, Mukalinzi 0, Muganza 3. Mikutano ya kijiji Muganza 1, Mukubu ulifanyika mkutano 1,Mukalinzi 0, Kamati ya Maendeleo ya Kata Muganza ulifanyika mkutano 1.

Hali ya ulinzi na usalama kwa kata ya Muganza ni nzuri kwani wananchi katika vijiji vyote wanafanya doria za usiku na viongozi wa vijiji wanasimamia zoezi hili la ulinzi na usalama kikamilifu.

**MUHT NA4/2015/2016: MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

**MAJIBU YA MASWALI YA PAPO KWA PAPO TOKA KWA WAHESHIMIWA MADIWANI KWENYE KIKAO CHA BARAZA TAREHE 3/12/2016.**

Katibu alisoma maswali ya papo kwa papo na majibu yake kama ifuatavyo;

NA.	MUULIZA SWALI	SWALI	JIBU
1	MHE. JOHN SHIMILIMANA  KATA YA KIBIMBA	Kuna viporo vingi ambavyo havikutekelezwa tangu Mwaka 2014/15 na 2015/16,hivi sasa tupo 2016/17. Je? Kuna mkakati gani wa kukamilisha Miradi hiyo? Mf. Ujenzi wa vyumba vya Madarasa S/M Ruganzo ‘B’, nyumba ya mganga Kumutana, na bweni la wanafunzi Shule ya Sekondari Kibimba.	Ni Kweli hadi sasa Halmashauri ina viporo vingi vya Miradi ambavyo havijakamilika katika Bajeti ya Mwaka 2014/15 na 2015/16.  Kwa kuwa hadi sasa fedha za miradi za Mwaka 2015/16 hazijapokelewa Halmashauri imeweka mkakati wa kuweka Miradi yote viporo kwenye Mpango na Bajeti wa Mwaka 2017/18 kwani ni Imani yetu kwamba tutaletewa fedha. Hivyo Miradi hiyo kama Madarasa S/M Ruganzo ‘B’, Nyumba ya mwalimu Kagali na Ntobeye, Nyumba ya Mganga Kumutana pamoja na Miradi mingine viporo itapewa kipao mbele.
2	MHE. MUKIZA S. BYAMUNGU  KATA -	Ni lini Hospitali ya Nyamiaga itatenga Wodi ya wagonjwa wa kawaida na wagonjwa wa majeraha?	Mganga Mkuu wa Wilaya amekwishatoa maelekezo kwa mganga Mkuu wa Hospitali kuwatenga wagonjwa na inafanyika hivyo tatizo ni pale ambapo hospitali haina majengo ya kutosha.

	MURUKULAZO		
3.	MHE. REHEMA S. RAMADHANI  KATA - MURUSAGAMBA	<p>a) Kwakuwa Mganga wa Kituo cha Afya Murusagamba anaumwa kila mara ni lini tutapatiwa Mganga mwingine ili waweze kutoa huduma ikizingatiwa kituo hicho kina upungufu pia wa wauguzi?.</p> <p>b) Aidha Mganga huyo ana tuhuma ya kuchukua fedha bila risti. Je ni hatua gani zitachukuliwa dhidi yake?</p>	<p>Mganga wa kituo cha Afya Murusagamba tayari amehamishiwa hospitali ya Rulenge na Daktari Mwingine toka hospitali ya Rulenge amehamishiwa Murusagamba, na baada ya siku 14 atapelekwa</p>
4	MHE. MUKIZA S. BYAMUNGU  KATA - MURUKULAZO	<p>Halmashauri ya Wilaya ni mionganini mwa Wilaya zinazozidi kukua hususani baadhi ya miji kupanuka na kuongezeka kwa watu, hivyo kuwepo mahitaji makubwa ikiwemo mahitaji ya makazi ya kudumu. Je ni wapi yametengwa makazi ya kudumu kwenye mji wa</p>	<p>Mji wa Ngara ni mamlaka ya Mji mdogo hivyo unatakiwa uwe na makazi ya kudumu na Mji upangwe vizuri.</p> <p>Halmashauri inaendelea kuandaa ramani za Mipango Miji kadri fedha zinapopatikana. Mwaka 2015/2016 tuliandaa TP ya Mkididiri na mwaka huu 2016/2017 shughuli hii iko kwenye bajeti lakini hatujapata fedha.</p>

		Ngara?	
5	MHE. KIIZA PHILBERT KATA - KASULO	<p>Katika Kata Kasulo ipo migogoro sugu ya ardhi. Kufuatilia agizo la Waziri Mkuu la kusitisha umiliki wa mashamba /ardhi zinazomilikiwa kinyume cha taratibu, kanuni na sheria, na bado agizo hilo halina utekelezaji hadi hivi leo. Pamoja na hilo, kuna ardhi zinazomilikiwa zaidi ya miaka 10 na wamiliki binafsi bila kufanyiwa maendelezo kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa wakati wanaomba ardhi hiyo lakini bado na masharti mengine ya mmiliki kwa mfano kutolipa ada ambao ni ukiukwaji wa masharti ya umiliki wa ardhi kwa muda mrefu.</p> <p>Je , ni lini Halmashauri itakamilisha taratibu za kurejesha mashamba hayo ili yawe na manufaa kwa wakazi wa wilaya ya Ngara hasa</p>	<p>(a) Mashamba 11 yaliyofutwa kwa kutozingatia taratibu kanuni na sheria za umiliki wa ardhi yako kwenye Kata ya Kasulo. Mashamba haya yanasmamiwa na yanagawanywa na kijiji kwa kuzingatia taratibu, Kanuni na sheria za kugawa na kumilikishwa ardhi. Kinachotakiwa kufanyika kwa kijiji cha Rwakalemela ni:-</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1. Kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi.</li> <li>2. Watu ambao hawana ardhi wapeleke barua za maombi kwenye Halmashuri ya kijiji zihadiliwe kwenye Serikali ya Kijiji na zipitishwe na Mkutano Mkuu wa Kijiji.</li> </ol> <p>(b) Mashamba 4 yenyе hati miliki za kamishna na hayaendelezwi inavyostahili. Wamiliki wa mashamba haya waliandikiwa Ilani ya kusudio la kuanza mchakato wa kufuta hati miliki za mashamba yao.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>- Ndugu Abdallah Sadallah hakupatikana na hajulikani aliko. Hivyo mchakato unaendelea wa kufuta hati miliki ya shamba lake no 235 ( na 208.18).</li> <li>- Ndugu Nyambele Mshengezi ambaye ana mashamba 2 No 745 (ha 198.9) na No 746 (ha 155.53) alileta barua ya kujitetea. Hivyo wataalamu wanatakiwa wakakague mashamba yake kujiridhisha kama uttezi wake ni sahihi.</li> </ul>

		wale wenye mapungufu / ukosefu wa ardhi?	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Ndugu Mahsein Said alileta barua ya kujitetea. Wataalamu wako kwenye zoezi la kukagua shamba lake No 333(HA 183.2) kujiridhisha kama utetezi wake ni sahihi.</li> </ul>
6.	MHE. JUSTUS K. MASUMO  KATA - NYAKISASA	a) Ni utaratibu upi unaotumika kupata watendaji wa muda?	<p>Watendaji wa muda wanapatikana kwa kuingia mkataba kati ya Menejimenti na Mtumishi husika.</p> <p>Aidha, ajira za watendaji wa vijiji zinategemea kibali cha Serikali na nafasi hizo kuwepo kwa Bajeti yake, kutokana na ufinyu wa fedha Serikali inatoa nafasi kidogo kidogo ndio maana sehemu zisizo na watendaji hulazimika kuweka watendaji wa Mkataba.</p>
		b) Watendaji wa muda wanapataje uhamisho toka Kata moja kwenda Kata nyingine au Tarafa nyingine?	<p>Watendaji wanahamishwa kutoka Kata moja kwenda nyingine kutokana na mahitaji na ulazima uliopo.</p>
7.	MHE. WILBARD BAMBARA  KATA - RUSUMO	Kwakuwa wakati wa kutenga Kata ya Rusumo Mwaka 2010 na kuzaliwa kata ya Kasulo kila Kata iliainihiwa vijiji vinavyounda Kata hizo na mojawapo ilikuwa Kata ya	<p>Serikali hutenga maeneo ya Utawala kulingana na uwezo uliopo, na uwezo wa eneo husika kukidhi vigezo vya kisheria ili kupewa hadhi ya Kijiji na Kata. Vigezo hivo ni kama idadi ya watu kati ya 3000 na 5000, idadi ya kaya zisizopungua 250 hadi 300, vitongoji visivopungua 5, uwezo wa viongozi na watumishi kuhudumia eneo</p>

		<p>Rusumo iundwe pamoja na vijiji vingine kikiwemo kijiji cha Kabulanzwili ambacho mpaka sasa hakitambuliki kwa mujibu wa sheria na kimebakki kikiwa kijiji cha Kasharazi ambacho ni kikubwa sana na Wananchi kutembea zaidi ya KM. 10 kutafuta huduma ya Ofisi ya Kijiji cha Kasharazi, je ni lini Kijiji hicho kitatambulika? Na serikali ilikuwa na maana gani Mwaka 2010 kutenga Kata? Na wananchi wangu niwambie nini kuhusu usajili wa kijiji hicho cha Kabulanzwili?</p>	<p>jipya la ki-utawala na uwezo wa Halmashauri kumudu gharama za ongezeko la maeneo ya ki-utawala</p> <p>Hata hivyo vijiji vyote na kata vilivyoombewa sio vyote vilivyokubaliwa ikiwemo kijiji cha Kabulanzwili.</p> <p>Itakapotolewa fursa tena na Serikali ya kugawa maeneo ya Utawala Kijiji cha Kabulanzwili kitaiingizwa katika orodha ya maeneo mapya ili kitengwe kwa lengo la kuwawezesha Wananchi kupata huduma kwa karibu.</p>
8	MHE. DAVID I. BUZUTU  KATA - MBUBA	<p>Watendaji wanao kaimu Ofisi za Vijiji wasio waajiriwa na kutolipwa mishahara, wanawezaje kukusanya mapato ya Halmashauri na makusanyo hayo yakawa mazuri?</p>	<p>a) Ni kweli Halmashauri ina Vijiji 13 ambavyo vina watendaji wanaokaimu kwenye Vijiji hivyo; Bulengo – Eliamani Hermani, Nyakiziba – Justus Lukaizakale, Kyenda – Mugisha Marcel , Ntobeye- Matatizo G. Gwishimpinga, Mukirehe Minani Bernado, Mubuhenge – Dawson B. Mazuru, Murutabo – Jared Elias, Mwivuza – Godwin Ladislaus, Ntanga – Onesmo Mayola, Kititiza – Minani J. Mwongele, Kashinka – Hamza J. Chabaye, Kanyinya – Mayala Kasunzu,</p>

			<p>Bukiriro – Nyabenda N. Rukonganya.</p> <p>b) Kukusanya mapato ni moja ya majukumu ya Mtendaji wa Kijiji, Aidha ni Mojawapo ya sharti la Mkataba wake wa kazi, anapokiuka mkataba taratibu za kisheria zinachukuliwa.</p>
9	MHE. CATHELINE M. EDWARD  VITI MAALUM - MURUSAGAMBA	<p>Kanuni ya vikao vya Halmashauri inaelekeza kuwa vikao vya kamati Kablasha, litawafikia wajumbe siku 3 kabla na Baraza la Madiwani siku saba kabla.</p> <p>a) Kwanini makablasha ya wajumbe yanapokelewa siku moja kabla au yanakutwa ukumbini? Je, kanuni imebadilika?</p> <p>b) Kama kanuni hajabadilika</p>	<p>Kanuni za vikao ziko palepale, makablasha yanatakiwa kuwafikia wahusika kama ilivyo elekezwa kwenye kanuni. Ila kutokana na changamoto za ukosefu wa fedha makablasha yanachelewa kuandaliwa ili yawafikie wahusika kwa wakati.</p> <p>Kanuni za vikao ziko pale pale makabasha yanatakiwa kuwafikia Wah. Mdiwani kwa wakati ila kuokana na changamoto za fedha kuna wakati inajitokeza makablasha yanachelewa.</p> <p>Aidha, ni lengo la Mkurugenzi kuhakikisha Wah. Wanapata makablsha kwa muda stahiki, isipokuwa zinapojitokeza changamoto zilizoelezwa hapo juu, Tunaomba radhi, suala hili halitajitokeza tena</p>

		kwanini utaratibu uliolekezwa haufuatwi?	
10	MHE. SUSANA B. NJOJOLO  VITI MAALUM – RULENGE	<p>a) Halmashauri ina mpango gani juu ya kutengeneza barabara ya Rwinyana - Nyabihungo ambapo mvua ikinyesha watoto wa shule wanahangaika na kushindwa kwenda shulenii.</p>	<p>Fedha za Mfuko wa barabara hutumika kufanya matengenezo ya barabara katika barabara zilizotambuliwa tu na si vinginevyo. Sheria ya barabara imezitambua barabara katika makundi kama ifuatavyo;</p> <p>a) Barabara Kuu  b) Barabara za Mikoa  c) Barabara za Wilaya  d) Barabara za Jamii</p> <p>Baada ya maelezo ya awali sasa naomba kutoa majibu kama ifuatavyo;</p> <p>i. Barabara iliyoulizwa iko katika kundi la Barabara zinazohudumiwa na jamii japo kuwa ilipasuliwa na mfuko wa DASIP. Halmashauri hapo nyuma iliweza kusaidia ujenzi wa Kalvalti tatu.</p> <p>ii. Uongozi wa Halmashauri unatoa wito kwa wanachi kuendelea kujitolea kufanya matengenezo ya barabara hii ili iweze kupitika, pia natoa ahadi ya kuona uwezekano wa kuiingiza barabara hii kwenye bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 pindi ukomo wa Bajeti utakapo ruhusu.</p>

		<p>b) Halmashauri ina mpango gani juu ya kutengeneza barabara ya Rwinyana - Nyabihungo ambapo mvua ikinyesha watoto wa shule wanahangaika na kushindwa kwenda shulenii.</p>	<p>Fedha za Mfuko wa barabara hutumika kufanya matengenezo ya barabara katika barabara zilizotambuliwa tu na si vinginevyo. Sheria ya barabara imezitambua barabara katika makundi kama ifuatavyo;</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>e) Barabara Kuu</li> <li>f) Barabara za Mikoa</li> <li>g) Barabara za Wilaya</li> <li>h) Barabara za Jamii</li> </ul> <p>Baada ya maelezo ya awali sasa naomba kutoa majibu kama ifuatavyo;</p> <p>iii. Barabara iliyoulizwa iko katika kundi la Barabara zinazohudumiwa na jamii japo kuwa ilipasuliwa na mfuko wa DASIP. Halmashauri hapo nyuma iliweza kusaidia ujenzi wa Kalvalti tatu.</p> <p>iv. Uongozi wa Halmashauri unatoa wito kwa wanachi kuendelea kujitolea kufanya matengenezo ya barabara hii ili iweze kupidika, pia natoa ahadi ya kuona uwezekano wa kuiingiza barabara hii kwenye bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 pindi ukomo wa Bajeti utakapo ruhusu.</p>
11	MHE. VAIETH MADENDE	Mkandarasi aliyejenga choo cha matundu mawili katika soko la Kanazi hafahamiki. Choo hiyo	Choo cha soko la Kanazi matundu mawili kilijengwa na Mkandarasi Gwaho CO. LTD kwa gharama ya shilingi 5,300,000, Mradi huo ulifanyiwa utekelezaji chini ya usimamizi wa ngazi ya Wilaya.

	VITI MAALUM.	imefungwa na imeanza kupata nyufa. Je? Ni lini choo hiyo itakabidhiwa ili ianze kutumika?	<p>Wakati wa makabidhiano ya choo kati ya Mkandarasi na Wataalamu wa Idara ya ujenzi, Mkandarasi alitakiwa au alielekezwa kurekebisha ufa uliotokea kwenye ukuta unaotenga matundu ya jinsia. Hadi sasa choo hicho kiko kwenye muda wa matazamio, ambapo mkandarasi hajalipwa Tshs. 265,000, hivyo basi ni matumaini yetu kuwa kabla ya kutoa malipo hayo ya matazamio mkandarasi atakuwa amefanya marekebisho hayo.</p> <p>Choo hiyo itatumika hadi sasa.</p>
12.	MH. ADRONIZ E. BURINDOLI	Kwa nini kuna vifo vyta mifugo hasa Ngómbe, vifo kama vya homa ya mapafu pamoja na ugonjwa wa miguu na midomo. Serikali yetu inajipangaje kudhibiti vifo hivyo kwa kutoa chanjo ya homa ya mapafu na ugonjwa wa miguu na midomo.	<p>Kuhusu udhibiti wa magonjwa ya</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>a) Homa ya mapafu kwa ngómbe</li> <li>b) Ugonjwa wa miguu na Midomo</li> </ul> <p>Haya magonjwa mawili ni mionganoni mwa magonjwa ya mlipuko amabyo yanatambulika kwamba yapo hapa nchini Tanzania.</p> <p>Utaratibu wa kuyadhibiti.</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1. Kutoa taarifa ya mlipuko wa ugonjwa na kuthibitisa</li> <li>2. Kuweka karantin baada ya kuthibitisha</li> <li>3. Kuchanja Ngómbe wote kila mwaka.</li> </ol> <p><b>KINACHOTOKEA HALI HALISI.</b></p> <p>Wizara ya mifugo na Uvuvi ndiyo yenye jukumu la kuagiza</p>

		<p>chanjo za magonjwa hayo lakini kwa muda mrefu hawajafanya hivyo.</p> <p>Hata hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imekuwa ikiweka kwenye bajeti kama tutapata fedha tutanunua chanjo na kuchanja.</p>
13.	<p>A. Ninaomba kujua jengo lililo kwenye soko la Kojifa ni lini litaanza kutumika? Kwa sababu wananchi wanauzia bidhaa zao chini hasa vyakula kama mboga na matunda hali hii kiafya siyo nzuri, meza zipo hazifanyi kazi kwa nini?</p>	<p>Jengo liliishakamilika muda mrefu takribani miaka miwili (2) iliyopita na liliisha kabidhiwa kwa Halmashauri.</p> <p>Matumizi ya jengo lile siyo kama ilivyotarajiwa kwa sababu kuu tatu (3).</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>i. Wananchi wameishajizoeza kuuzia bidhaa zao kwenye vichanja kiasi kwamba inahitajika nguvu ya ziada kuwatoa pale kwenye vichanja kwenda kuuzia kwennye vimeza ndani ya jingo la Soko.</li> <li>ii. Idadi ya wananchi wanaohitaji/ kupaswa kwenda kuuzia bidhaa zao kwenye vimeza ni kubwa kuliko idadi ya vimeza vilivyopo kwenye jingo la soko. Hii linaleta uzito wa kuamua nani ahamishwe kutoka chini kwenye vichanja kwenda kwenye jingo la soko na nani aachwe kwani Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo alishawahi kuwahamisha baadhi ya wafanya biashara kutoka kwenye vichanja kwenda</li> </ul>

		<p>kupanga bidhaa zao juu ya vimeza kwenye jingo la soko na matokeo ni kwamba waliohamishwa kwenye vimeza siku hiyo hawakufanya biashara kwani wateja wao wameshazoea kununua bidhaa zao kwenye vichanja vilivyopo chini ya jingo la soko.</p> <p>iii. Suala la usafi kwenye makabati ya vimeza vilivyopo kwenye jingo na jingo lenyewe kwa ujumla ni changamoto kwani soko lile halina ulinzi hivyo kufanya wachafuzi kuchafua soko kwa uhuru mkubwa.</p> <p>Hivyo kwa changamoto hizo basi, ndio inapelekea matumizi ya jingo la soko kuwa magumu na yenye changamoto kubwa na kwa hilo inakuwa vigumu kutamka moja kwa moja kwamba ni lini jingo lile litaanza kutumika.</p> <p>Jibu: Ni kweli kipindi hiki ni cha mvua hivyo sasa ombi la kuweka turubai (shitingi) pale kwenye jingo la mabomba lilipo kwenye soko la kojifa tunalichukua na tutalifanyia kazi.</p>
	Kipindi hiki cha Mvua tunaomba	

		tuwekewe shitingi kwenye yale mabomba ili wananchi wasinyeshewe.	
--	--	--	--

## **MUHT NA 5/2016/2017: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA**

Wajumbe walifanya masahihisho yafuatayo;

- *Jina la Suzana Bahati lisomeke Suzana N. Bahati*
- *Neno Mukuu lisomeke Mkuu*
- *Neno Nhi lisomeke Nchi*
- *Neno Kikao lisomeke Vikao*
- *Tarakimu 124440 lisomeke 12440*
- *Neno Murugunga lisomeke Murugina*
- *Neno Walijikubali lisomeke Waliojikubali*
- *Neno Maghairibi lisomeke Magharibi*
- *Neno Phyizikia lisomeke Fizikia*
- *Neno Mujebwe lisomeke Munjebwe*
- *Neno Kangati lisomeke Kazingati*
- *Neno Rujuba lisomeke Ruhuba*
- *Neno Kabanga lisomeke Kasulo*
- *Neno Waalimu lisomeke Walimu*
- *Maambukizi ya ugonjwa wa VVU lisomeke Maambukizi ya VVU*

## **MUHT NA 6/2016/2017: TAARIFA YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**

Mwenyekiti alitoa taarifa kuwa walihudhuria katika kikao cha ALAT Taifa na walitegemea Mgeni rasmi angekuwa Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania John Joseph Pombe Magufuli lakini kutokana na majukumu aliwakilishwa na Mhe. Simba Chawene hivyo katika kikao kile walimuomba Mhe. Simba Chawene kulifanyia kazi suala la posho za Waheshimiwa Madiwani na pia walimueleza kwamba fedha za utekelezaji wa miradi haziletwi hivyo miradi mingi hajatekelezwa hivyo fedha hizi zingeletwa ili kuweza kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi na Mhe. Simba Chawene aliahidi kulifikisha kwa Mhe. Rais ili yaweze kutekelezwa.

Aidha alileza kwamba walihudhuria katika kikao LOVELUCK na katika kufanya kikao hicho waliweza kufanya usafi katika hospitali 2 na kuweza kutoa magodoro 6, na tangu LOVELUCK imeanza inatimiza miaka 20 na kikao cha LOVELUCK kitafanyika katika nchi ya Uganda.

Vikao vya RCC jambo lililositisizwa ni Wakurugenzi Watendaji kuandaa maeneo ya kuhifadhi mifugo na walihoji kuhusu masuala ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na walijibowi kwamba fedha hizo zitaanza kuleta kuanzia mwezi Desemba, 2016

Walihudhuria semina tarehe 2/11/2016 kwa ajili ya upuliziaji wa ukoko, alisema kwamba dawa hiyo itapulizwa katika Wilaya 3 Bukoba DC, Ngara na Misenyi kwa Wilaya ya Ngara Waheshimiwa Madiwani waliombwa kutopeleka majina ya watu wao bali kila mtu atume maombi na waliahidi kila kijiji watachukuliwa watu 4

Alihudhuria katika kikao cha kazi na maagizo yaliyotolewa ni kuwa taarifa za Mkaguzi wa Ndani kupelekwa kwa wakati na hoja kujibiwa kwa wakati ikiwa ni pamoja na hoja za CAG kujibiwa kwa wakati.

Walienda Mkoani kupelekwa matokeo ya darasa la 7, alimpungeza Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Afisa Elimu Msingi kwa sababu Wilaya ya Ngara imekuwa ya 1 Kimkoa nay a 12 Kitaifa, shule ya msingi Kabanga imekuwa ya 1 na imetua watoto 3 kwenda kusoma katika shule maalumu, ikifuatiwa na shule ya msingi Mbwilinde imetua watoto 2 kwenda kusoma nje ya Mkoa.

Aidha alisema kwamba yapo maelekezo yaliyotolewa walipokwenda katika kikao cha LAAC-Dodoma na maelekezo hayo yatatolewa katika vikao vya kisheria vitakavyofanyika, alimuomba Mkurugenzi Mtendaji Kufuatilia maelekezo yote yaliyotolewa ili yaweze kufanyiwa kazi.

#### **MUHT NA 7/2016/2017: TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

Mkurugenzi Mtendaji alisema kwamba katika kutekeleza majukumu yake alihudhuria vikao mbalimbali vya kisheria na Wataalam ili kuweza kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Katika kupunguza gharama za matengenezo ya magari ya Halmashauri, matengenezo kufanyika mpaka gari kupelekwa TEMESA suala hili lilijadiliwa na kuchukuliwa na Waziri mwenye dhamana na aliahidi kwenda kulifanya kazi na atatoa mwongozo mpya juu ya matengenezo ya magari ya Halmashauri.

Pia alihudhuria kikao cha barabara, katika kikao ziliibuliwa hoja mbalimbali na hoja ilioigusa Halmashauri ilikuwa ni suala la manunuzi, ilionekana kwamba Maafisa Ugavi pamoja na Waheshimiwa Madiwani kutumia makampuni yao katika kutekeleza miradi na kutofuta sheria za manunuzi hivyo ilielekezwa kwamba haitaruhusiwa kwa Maafisa Ugavi pamoja na Waheshimiwa Madiwani au Wataalam kwa ujumla kupelekwa makampuni yao kwa ajili ya kupata tenda za barabara au kazi yoyote itakayotangazwa na Halmashauri.

Mkurugenzi Mtendaji alisema kwamba kuna baadhi ya Maafisa Ugavi kutoa tenda vivuli na badala yake tenda hizo kuwa za kwao, alitoa mfano wa Mkandarasi aliyepewa tenda ya kushona sare za shule alipofuatiwa kwanini hakamilishi kazi kwa wakati iligundulika Mkandarasi huyo alipewa maelekezo na Afisa Ugavi kuwa atampa ushirikiano katika

kumpatia vifaa vya kutengenezea sare, alitoa onyo kwa Maafisa Ugavi kuacha kutoa tenda vivuli na kama suala hilo litajirudia atakayehusika attachukuliwa hatua.

Aidha aliongeza kwamba ukiukwaji wa sheria unaofanywa na Bodi ya Zabuni, ilielekezwa kwamba atakayepewa tenda anatakiwa kuwa na mtaji utakaowezesha kazi kufanyika na kukamilika na suala hilo ameliona hata kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kwamba kuna baadhi ya Wakandarasi wanapewa kazi na kushindwa kuzikamilisha au kushindwa kulipa vibarua, hivyo ilishauriwa kama Mkandarasi hatakuwa na uwezo wa kifedha asipatiwe tenda/kazi. Pia Wakandarasi wanatakiwa kuwa na mashine za EFD na kama hawatakuwa na mashine hizo waondolewe moja kwa moja, aliongeza kwamba baada ya kutolewa kwa tangazo hilo baadhi ya Wakandarasi wameanza kununua mashine za EFD.

Suala la miradi ya maendeleo, katika kutekeleza hilo aliwashukuru Waheshimiwa Madiwani ambao wanatoa mikakati mbalimbali katika kufanikisha ujenzi wa eneo la maegesho ya magari lililoko Benaco-Kasulo na endapo ujenzi utakamilika Halmashauri itakusanya Tshs. 70,000,000/= kwa mwezi hatua iliyofikiwa mpaka sasa eneo limefanyiwa usafi (clearance) lakini ilijitokeza changamoto iliyopelekea usafi (clearance) wa eneo kutofanyika kwa wakati, aliahidi kufanya ufuatiliaji na kulifanyia kazi.

Katika kikao cha RCC waliagizwa kuwabdalisha vyeo Watumishi wenye sifa mfano kuna Watumishi wenye sifa za kuwa Maafisa Misitu na walishaomba hivyo aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kutoa matangazo katika vikao vya WDC kama kuna Watumishi wenye taaluma mbalimbali watume maombi katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ili waweze kubadilishwa vyeo.

Aidha alieleza kwamba kama Mwenyekiti wa Halmashauri alivyotoa taarifa walihudhuria katika kikao cha upuliziaji na ukoko kwa ajili ya kuzuia malaria majumbani, aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kuweka matangazo mapema yanayohusu upuliziaji ukoko ili wananchi watakaokiuka/ kupinga nguvu ya dola itumike.

#### **MUHT NA 8/2016/2017: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA II 2016/17**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa ya utekelezaji. Wajumbe walipokea tarifa na kuijadili. Mjumbe mmoja alihoji kuhusu fedha za CEDEP, kwa sababu walitembelea mradi wa Nyakisasa na kukuta nyumba za mradi hazijakamilika, aliataka kufahamu kama fedha hizi vado zipo ama la?.

Katibu alisema kwamba Mkandarasi anayejenga shule ya sekondari Nyabisindu ndiye aliyeju na tuhuma za kwamba fedha za mradi zimetumika kwenye kazi nyingine, alisema fedha zipo ila Mkandarasi alikuja na tuhuma hizo kwa sababu aliambiwa abomoe baadhi ya sehemu ya majengo kwa kuwa hazikuwa na ubora wa kutosha, Mkandarasi atakapomaliza kazi atalipwa fedha zake.

Mjumbe mwingine alihoji juu ya gari la TASAF alisema kwamba taarifa kuhusu uharibifu wa magari huletwa katika vikao husika alihoji kwanini taarifa kuhusu gari la TASAF hazijawasilishwa katika kikao?

Katibu alisema kwamba ni kweli gari la TASAF lilipata ajali likitokea kwenye msiba wa mzazi wa Mtumishi Bw. Julius Moringo, Halmashauri ilishatoa taarifa TASAF Makao Makuu na muda si mrefu gari litaanza kufanya kazi, hii ni kwa sababu Mtumishi mwenyewe ndiye aliyetumia gharama zake binafsi kulifanyia matengenezo gari hilo

Mjumbe mmoja alitaka kufahamu kwanini kazi zingine za barabara hazitangazwi, Afisa Ugavi alijibu kwamba kazi zinazozidi milioni 200 ndizo zinazopaswa kutangazwa kisheria, zilizo chini ya hapo ofisi inatumia Quation kupata Wakandarasi.

Mjumbe mwingine alishauri katika kikao cha Kamati ya fedha, utawala na mipango kinachokuja wajumbe wapatiwe utaratibu mzima wa ugawaji wa tenda kwa wakandarasi.

Mjumbe mmoja alihoji kama Mkurugenzi anapata taarifa zozote toka katika kitengo cha Ugavi, Afisa Ugavi alijibu kwamba taarifa zote hupelekwa katika tender Board na kama kuna tatizo lolote ambalo litajitokeza ndipo Mkurugebzi Mtendaji atahusishwa.

Mjumbe mwingine alisema kwamba shughuli zote za Halmashauri zipo chini ya Mkurugenzi Mtendaji hivyo kila kinachofanyika lazima taarifa ipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji na baada ya Mkurugenzi Mtendaji kupata taarifa atatakiwa kuwasiliana na Mwenyekiti wa Halmashauri ambae nae atapeleka taarifa kwa Waheshimiwa Madiwani Mwenyekiti alisema kwamba hatasaini mikataba ya Wakandarasi ambao wanadaiwa fedha na vibarua

#### **MAAZIMIO:**

1. Fedha za madawa zirudishwe ifikapo ntarehe 17/12/2016
2. Afisa Ugavi awasilishe utaratibu na kanuni za utangazaji na ugawaji wa tenda kwenye kikao cha Kamati ya fedha utawala na mipango kijacho
3. Kabla ya kikao Afisa Ugavi awasilishe fomu inayowatambulisha Wakandarasi wote wanaopewa tenda na Halmashauri

Baada ya majadiliano wajumbe waliipitisha taarifa .

#### **MUHT NA 9/2016/2017: TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU**

#### **KAMATI YA FEDHA UTAWALA NA MIPANGO**

Makamu Mwenyekiti aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango Wajumbe walipokea taarifa na kuipitisha, baada ya kuwasilisha aliwashukuru wajumbe kwa kuipokea taarifa.

## **KAMATI YA UJENZI UCHUMI NA MAZINGIRA**

Mwenyekiti wa kamati aliwasilisha taarifa. Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili. Mjumbe mmoja alisema kwamba Watendaji wa Kata wamekuwa hawapatiwi 10% wanapowasilisha fedha Halmashauri, je Mwenyekiti wa Kamati anawahakikishia nini wajumbe juu ya malalamiko yanayotolewa na Watendaji wa Kata? Mwenyekiti wa kamati alijibu kwamba kuna Kamati nmaalumu ya kukusanya mapato ya Halmashauri tofauti na makusanyo yanayofanywa na Watendaji wa Kata na kamati hiyo maalumu ilishapatiwa gari, ni kweli Watendaji waliomba kupatiwa 10% ya makusanyo yanayowasilishwa Halmashauri, katika kulifanyia kazi suala hilo Mkurugenzi Mtendaji ameongeza kiasi cha makusanyo anachotakiwa kuwasilisha Mtendaji wa Kata toka Tshs. 2,000,000/= na zaidi ili waweze kupatiwa 10% walizoomba. Ilisiaazimiwa kila Mheshimiwa Diwani katika vikao vya Chama kufika na taarifa makusanyo ya fedha ya miezi 3 ya Kata.

Mjumbe mwengine alihoji kama eneo la ofisi za Halmashauri (Makao Makuu) limeshapimwa na kupatiwa hati, Mwenyekiti alijibu kwamba wajumbe wawe na subira kwa sababu kuna maazimio yalitolewa katika kikao kilichopita kuhusu upimaji wa viwanja hivyo taarifa itawasilishwa katika kikao kijacho cha Baraza la Madiwani. Wajumbe waliipitisha taarifa na baadae Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuipokea taarifa kuipitisha.

## **KAMATI YA ELIMU AFYA NA MAJI**

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa. Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili. Mjumbe mmoja alimuomba Mwenyekiti wa Kamati ya elimu, afya na maji kutembelea katika kituo cha afya Murusagamba ili kuona mapungufu yaliyoko katika kituo kile kwa sababu kuna Watumishi zaidi ya 3 wameshamishwa.

Mwenyekiti alijibu kwamba ushauri umezingatiwa wanasubiri kibali cha ajira ambapo waliahidiwa zaidi ya Watumishi 66 hivyo wajumbe wawe na subira, Wajumbe waliipitisha taarifa na baadae Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuipokea taarifa kuipitisha.

## **KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI (CMAC)**

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilsha taarifa, Wajumbe waliipokea taarifa na kuipitisha na baadae aliwashukuru wajumbe kwa kupokea taarifa.

## **NENO LA SHUKRANI TOKA KWA M/KITI WA CCM**

Mwenyekiti wa CCM alianza kwa kuwasalimia wajumbe na kuzungumzia mabo yafuatayo; Baada ya kufanya uchaguzi tarehe 25/01/2015 na Chama cha Mapinduzi kuibuka mshindi kuna baadhi ya Watendaji walisema kwamba Baraza la Chama kimoja haliwezi kufanya

kazi, lakini kazi inayofanyika inaonekana na kuwasihii Waheshimiwa Madiwani kutokuwa na woga.

Alimuomba Mkurugenzi Mtendaji kuzingatia ratiba za vikao kama vikao hivyo havitakuwa na sababu ya kuhairishwa.

Kipengele cha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupewa nafasi kubwa na taarifa isomwe kwa uwazi, alishukuru maamuzi yaliyotolewa na kuwaomba Waheshimiwa Madiwani kutokubali majibu yasiyo na mashiko toka kwa Wataalam, na kuwashukuru wajumbe kwa kumsikiliza.

### **MUHT NA 10/2016/2017: TAARIFA YA UTUMISHI NA UTAWALA**

Makamu Mwenyekiti alisema kwamba kulingana na kanuni ya 39, Baraza linapaswa kujibadilisha na kuwa Kamati ili kuweza kujadili masuala ya kiutumishi.

Mwenyekiti alikubaliana na suala hilo na Baraza lilijibadilisha na kuwa Kamati.

Afisa Utumishi aliwasilisha taarifa. Wajumbe waliipokea taarifa.

Mwenyekiti alitoa ufanuzi kwa wajumbe ambao sio wajumbe wa Kamati ya fedha, utawala na mipango kuwa suala linalojadiliwa ni la msitu wa Lumasi, alieleza kwamba Kamati ya fedha, utawala na mipango iliona kwamba watumishi hao hawafai kuwa watumishi wa Halmashauri hivyo ni vyema wakafukuzwa kazi.

Mjumbe mmoja alihoji kama watumishi watafukuzwa kazi watarudisha fedha walizoipatia hasara Halmashauri Tshs. 271,000,000/= baada ya kufukuzwa kazi?

Mjumbe mwengine alisema kwamba wajumbe kwa kauli moja wakubaliane kuwa watumishi hao waweze kufukuzwa kazi hivyo baada ya Baraza la Madiwani Mwenyekiti anapaswa kuwaita waandishi wa habari na kuwatangazia hatua zilizochukuliwa.

Baada ya majadiliano, Wajumbe wote kwa kauli moja walikubaliana watumishi hao Bw. Philip Ileta pamoja na Bw. Gwassa Kadende wafukuzwe kazi na Mwenyekiti alimuomba Mhe. John E. Ruzige kuwasilisha taarifa kwa niaba ya Wajumbe wa Baraza la Madiwani na aliwasilisha kama ifuatavyo;

**A.**

- Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Nfara lililokutana tarehe 3/12/2016 limejadili shauri la kinidhamu la Bw. Philip Ileta na Bw. Gwassa Kadende.
- Baraza limepokea maoni na mapendeleko yaliyotolewa na TUME YA UCHUNGUZI iliyoundwa na Katibu Tawala wa Mkoa Kagera ambayo imejiridhisha kuwa tuhuma zinazowakabili watuhumiwa hao zimethibitika bila shaka.
- Kwa kauli moja Baraza la Madiwani leo tarehe 3/12/2016 limeazimia yafuatayo;
  1. Bw. Philip Ileta(Afisa Misitu) na Bw. Gwassa Kadende (Msaidizi wa Misitu) wafukuzwe kazi kuanzia leo kwa kuisababishia Halmashauri ya Wilaya ya Ngara hasara ya kiasi cha Tshs. 271,670,000/= katika uvunaji wa msitu wa

Lumasi na Lukole katika kipindi cha Aprili 2012 hadi Novemba 2014. Hii ni kwa kuzingatia kanuni za Utumishin wa Umma za mwaka 2003, kanuni namba 42.

Aidha Baraza linaazimia walinzi wawili (Bw. Nicoulaus Andrew na Bw. Geofrey Biziman) wanaotuhumiwa kushiriki katika ubadhilifu wa msitu wa Lumasi na Lukole mchakato wa kuchukulia hatua za kinidhamu kwa mujibu wa kanuni za Utumishi wa Umma uanze rasmi na taarifa za utekelezaji ziletwe katika kikao cha Baraza la Madiwani kijacho

**B.**

- Baraza la Madiwani limeazimia kumfukuza kazi Bi. Pendo Antony( Mhudumu wa Afya Kituo cha Afya Nyamiaga) kwa kosa la kutokuwepo kazini bila likizo wala ruhusa ya kutoka kwa Mwajiri kwa zaidi ya siku 5 mfululizo.
- Baraza limezingatia kifungu cha sheria namba 42(1) cha kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003

**MUHT NA 11/2016/2017: TAARIFA YA MASUALA YA KISHERIA**

Taarifa ya masuala ya kisheria haikuwepo kwenye agenda, hivyo agenda hiyo haikujadiliwa.

**NENO LA SHUKRANI TOKA KWA MKUU WA WILAYA**

Mkuu wa Wilaya alisema kwamba kumekuwepo na changamoto ya kuwepo kwa ndoa za utotonu na kesi hiyo kuwasilishwa katika kikao cha ulinzi na usalama, aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kushirikiana katika kukomesha suala hilo

Suala la imani potofu, vikongwe wamekuwa wakiuwawa kwa kuhusishwa na imani za kishirikina wakati watu wanakufa kutokana na magonjwa mbalimbali, alishauri elimu itolewe kwa wananchi juu ya masuala ya imani potofu inapotokea mtu anaugua ni vyema akapelekwa hospitalini mara moja na sio kwa waganga wa kienyeji.

Suala la Watumishi kufanya kazi kwa mazoea, alishauri watumishi kuacha kufanya kazi kwa mazoea, kila mtumishi ajitahidi kufanya kazi na kutoa huduma inapohitajika kwa wananchi pia kutoa maelezo yaliyo sahihi kadri ya uelewa wa huduma, alipongeza kwa hatua zilizochukuliwa kwa watumishi wote wanaokikuka maadili ya kazi.

**MUHT 12/2016/2017: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote waliohudhuria kikao na kwa maamuzi magumu yatatolewa na kuongeza mambo yafuatayo;

1. Hawatafumbia macho kiongozi yejote atakayekiuka taratibu za Kiutumishi na kutoa mfano wa Mtendaji wa Kata aliyehamishwa Katika Kata ya Kabanga na kupelekwa Nyamagoma wakati anadaiwa fedha za wananchi, kikao cha Kamati ya fedha, utawala na mipango kiliazimia Mtumishi huyo kufukuzwa kazi.
2. Uhamasishaji ufanyike kwa watoto wote walioshinda mitiani na kupelekwa kidato cha kwanza kama ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyosema na wazazi wote watakaokiuka au kukataa wapelekwe mahakamani.

3. Wakandarasi wote wanaoomba kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara walipe posho za vibarua, kupitia hadhara hii kama watashindwa hawatapatiwa kazi tena na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.
  4. Aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kusaidia katika suala la ukusanyaji wa mapato kwa sababu kumekuwa na hujuma kwa wanaokusanya ushuru na Watendaji wote wanaofanya hivyo watawajibishwa.
  5. Katika kipindi hiki cha sikukuu aliwaomba wananchi kuacha walinzi majumbani wanapokwenda katika ibada za usiku.
  6. Kupitia kikao cha Baraza la Madiwani wanawapongeza watoto wote walioshinda mitiani ya darasa la saba
  7. Kuhusu upatikanaji wa eneo la maziko kwa ajili ya watu wa dini zote, alimuumba Mkurugenzi Mtendaji na Afisa Ardhi ili kuweza kutenga eneo hilo.

Kikao kilifungwa saa 8.10 mchana.

UMETHIBITISHWA

Mh. Erick Nkilamachumu Bw. Aidan J. Bahama

# MWENYEKITI

KATIBU

**Tarehe...../.....2017**